

جمهورية تنزانيا الاتحادية
JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
وزارة التربية والتعليم والعلوم والتكنولوجيا
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA



مقرر اللغة العربية للمرحلة الثانوية العامة
الصف IV-I

MUHTASARI WA LUGHA YA KIARABU
ELIMU YA SEKONDARI KIDATO CHA I-IV
2023

© مؤسسة تنزانيا للتربية؛ 2023م
الطبعة الأولى 2023م
رقم ISBN 978-9987-09-833-0

مؤسسة تنزانيا للتربية

ص.ب 35094

دار السلام؛ تنزانيا

رقم الهاتف: +255 735 041 168 / 735041170

بريد إلكتروني : director.general@tie.go.tz

موقع إلكتروني: www.tie.go.tz

ينبغي توثيق هذا المقرر على النحو التالي: وزارة التربية والتعليم والعلوم والتكنولوجيا. (2023م). مقرر اللغة العربية للمدارس الثانوية العامة من الصف الأول الثانوي إلى الصف الرابع الثانوي. مؤسسة تنزانيا للتربية.
جميع الحقوق محفوظة. لا يجوز إعادة إنتاج المقرر أو تخزينه في أي نظام استرجاعي أو نقله أو تفسيره بأي شكل أو بأية طريقة دون إذن مسبق من مؤسسة تنزانيا للتربية

© Taasisi ya Elimu Tanzania, 2023
Toleo la Kwanza, 2023

ISBN: 978-9987-09-833-0

Taasisi ya Elimu Tanzania
S.L.P 35094
Dar es Salaam, Tanzania

Simu: +255 73 5041 168 / 735 041 170
Barua pepe: director.general@tie.go.tz
Tovuti: www.tie.go.tz

Muhtasari huu urejelewe kama: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (2023). *Muhtasari wa Lugha ya Kiarabu Elimu ya Sekondari, Kidato cha I-IV*. Taasisi ya Elimu Tanzania.

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha, kutafsiri wala kutoa muhtasari huu au sehemu yake kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania.

المحتويات

Yaliyomo

vi	قائمة الجداول:
vi	Orodha ya Majedwali
vii	قائمة الملخصات
vii	Vifupisho
viii	الشكر والتقدير
ix	Shukrani
1	1.0 المقدمة
1	1.0 Utangulizi
1	2.0 الأهداف الرئيسية للتعليم في تنزانيا
1	2.0 Malengo Makuu ya Elimu Tanzania
4	3.0 أهداف التعليم للمرحلة الثانوية العامة
4	3.0 Malengo ya Elimu ya Sekondari Kidato cha I–IV
5	4.0 المهارات العامة للتعليم الثانوية العامة
5	4.0 Umahiri wa Jumla wa Elimu ya Sekondari Kidato cha I–IV
6	5.0 الكفاءات العامة و الكفاءات الخاصة
6	5.0 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi
8	6.0 دور المعلمين والطلاب والآباء في تعليم وتعلم

86.0 Majukumu ya Mwalimu, Mwanafunzi na Mzazi/Mlezi katika Ufundishaji na Ujifunzaji
9المعلم 6.1
96.1 Mwalimu
11الطالب 6.2
116.2 Mwanafunzi
12 الوالد / الوصي 6.3
126.3 Mzazi/Mlezi
13أساليب التدريس المقترحة 7.0
137.0 Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji
138.0 الوسائل التعليمية المقترحة
138.0 Zana za ufundishaji na ujifunzaji
14قياس تقدم التعلم 9.0
149.0 Upimaji wa Maendeleo ya Ujifunzaji
16عدد الحصص 10.0
1610.0 Idadi ya Vipindi
16محتوى التعليمية والتعلمية 11.0
1611.0 Maudhui ya Ufundishaji na Ujifunzaji
82قائمة المراجع :
82Bibliografia

قائمة الجداول:

6	الجدول رقم 1 : الكفايات العامة والكفايات الخاصة
15	الجدول رقم 2 : توزيع علامات التقييم
17	الجدول رقم 3 : محتوى الصف الثانوي I
32	الجدول رقم 4 : محتوى الصف الثانوي II
48	الجدول رقم 5 : محتوى الصف الثانوي III
66	الجدول رقم 6 : محتوى الصف الثانوي IV

Orodha ya Majedwali

Jedwali Na 1: Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi	6
Jedwali Na 2: Mgawanyo wa Alama za Upimaji	15
Jedwali Na 3: Maudhui ya Kidato cha I	17
Jedwali Na 4: Maudhui ya kidato cha II	32
Jedwali Na 5: Maudhui ya Kidato cha III	48
Jedwali Na 6: Maudhui ya Kidato cha IV	66

قائمة الملخصات

TET	مؤسسة تنزانيا للتربية
TEHAMA	تكنولوجيا المعلومات والاتصالات
LAT	لغة الإشارة في تنزانيا

Vifupisho

TET	Taasisi ya Elimu Tanzania
TEHAMA	Teknolojia ya Habari na Mawasiliano
LAT	Lugha ya Alama Tanzania

الشكر والتقدير

الشكر والتقدير

شارك في إعداد مقرر اللغة العربية للمرحلة الثانوية العامة لصف IV-I خبراء متنوعين من المؤسسات الحكومية وغير الحكومية. تود مؤسسة تنزانيا للتربية (TET) أن تتقدم بخالص الشكر والتقدير لجميع هؤلاء المتخصصين الذين ساهموا في تطوير هذا المقرر. بالإضافة إلى ذلك ، تقدم TET شكرًا خاصًا للمحاضرين والمدربين ومراقبي جودة الشاملة للمدارس ومطوري المناهج من TET. كما تتقدم المؤسسة الشكر و التقدير للجنة الفنية الوطنية التي عينها وزير التربية والتعليم والعلوم والتكنولوجيا للإشراف على عملية مراجعة المناهج لمرحلة الأساسية والابتدائية والثانوية وتدريب المعلمين. وفت اللجنة بالتزاماتها بطريقة احترافية من خلال التأكد من أن هذا المقرر يزود الخريجين بالمهارات والمعرفة التي تمكنهم من العمل لحسابهم الخاص ، والتوظيف، والقدرة على إدارة حياتهم اليومية، وهو ما يتماشى مع الهدف الأساسي لمراجعة المناهج الدراسية لعام ٢٠٢٢م أخيرًا، تتقدم TET شكرًا خاصًا لوزارة التربية والتعليم والعلوم والتكنولوجيا لتسهيل إعداد وتوزيع هذا المقرر



Dkt. Aneth A. Komba

المديرة العامة

مؤسسة تنزانيا للتربية

Shukurani

Maandalizi ya Muhtasari wa Lugha ya Kiarabu Elimu ya Sekondari kidato cha I-IV yamehusisha wataalamu mbalimbali kutoka taasisi za serikali na zisizo za serikali. Taasisi ya Elimu Tanzania (TET), inatambua na kuthamini michango ya washiriki wote waliofanikisha kupatikana kwa muhtasari huu. Aidha, TET inatoa shukurani za pekee kwa wahadhiri, wakufunzi, wathibiti ubora wa shule, walimu pamoja na wakuza mitaala. Vilevile, TET inaishukuru kwa dhati Kamati ya Kitaifa ya Wataalamu kwa Kusimamia Kazi ya Maboresho ya Mitaala ya Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Ualimu iliyoteuliwa na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia. Kamati hii ilifanya kazi kwa weledi na kuhakikisha kuwa maudhui ya muhtasari huu yanalenga kuwaandaa wahitimu wenye maarifa, ujuzi na mwelekeo utakaowawezesha kujiajiri, kuajiriwa na kumudu maisha yao ya kila siku, ambalo ndio lengo kuu la maboresho ya mitaala ya mwaka 2023.

Mwisho, TET inatoa shukurani za pekee kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kuwezesha uandaaji na usambazaji wa muhtasari huu.



Dkt. Aneth A. Komba

Mkurugenzi Mkuu

Taasisi ya Elimu Tanzania

1.0 المقدمة

اللغة العربية مادة اختيارية في المرحلة الثانوية العامة لصف IV-I. الهدف من تعليم هذه اللغة هو تمكين الطالب من القدرة على الاستماع والتحدث والقراءة والكتابة باللغة العربية ، وبناء القدرة على استخدام اللغة بسهولة وفقاً لاحتياجات الاتصال في سياقات مختلفة. تفتح هذه اللغة العديد من الفرص بما في ذلك أن تكون موظفًا أو توظيف. كما سيمكن هذا الدرس التلميذ من إتقان المهارات الأساسية لمقارنة مفردات اللغة العربية وقواعدها باللغات الأخرى.

تم إعداد هذا المقرر بهدف إرشاد المعلم في تعليم وتعلم اللغة العربية من الصف الثالث إلى السادس في تنزانيا. يوضح هذا المقرر منهج التعليم الابتدائي لعام 2023م. بالإضافة إلى ذلك ، يمكن المقرر المعلم من تخطيط أنشطة التعليم والتعلم من خلال بناء مهارات التلميذ المتمثلة في الفضول والإبداع والتعاون والتواصل وحل التحديات في بيئته.

1.0 Utangulizi

Lugha ya Kiarabu ni somo chaguzi katika ngazi ya Elimu ya Sekondari Kidato cha I-IV. Lengo la kufundisha somo hili ni kukuza stadi za lugha ya Kiarabu za kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika ili kumjengea uwezo mwanafunzi wa kuwasiliana katika miktadha mbalimbali. Vilevile, mwanafunzi ataweza kutoa huduma za jamii kwa kutafsiri, kuhariri na kukalimani mazungumzo sahili, hivyo, kuweza kumudu maisha yake ya kila siku kwa kujiajiri na kuajiriwa. Vilevile, somo hili litamwezesha mwanafunzi kumudu utunzi wa matini mbalimbali kwa lugha ya kiarabu.

Muhtasari huu umeandaliwa kwa lengo la kumwongoza mwalimu katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiarabu . Muhtasari huu ni mwendelezo wa Muhtasari wa Lugha ya Kiarabu Elimu ya Msingi Darasa la III–VI ambao unazingatia mkabala wa kimawasiliano na unasisitiza kukuza stadi nne za lugha ambazo ni kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika. Vilevile, muhtasari unatoa nafasi kwa mwalimu kutumia mbinu mbalimbali za ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiarabu ili kumjengea mwanafunzi stadi za udadisi, ubunifu, ushirikiano, mawasiliano na utatuzi wa changamoto katika mazingira yake.

2.0 الأهداف العامة للتعليم في تنزانيا

من خلال توفير التعليم في تنزانيا، تتمثل الأهداف الرئيسية في تمكين كل تنزاني من:

- أ. تطوير شخصيته وتحسينها حتى يقدر على احترام نفسه ويثق بنفسه؛
- ب. احترام ثقافة تنزانيا وتقاليدها وعاداتها والاختلافات الثقافية والتراحم وحقوق الإنسان؛ والاتجاهات والتصرفات العامة؛
- ج. زيادة المعرفة واستخدام العلوم والتكنولوجيا والإبداع والتفكير النقدي والابتكار والتعاون والاتصال والاتجاهات الإيجابية من أجل تنميته والتنمية المستدامة للأمة والعالم بأسره؛
- د. فهم وحماية القيم الوطنية، بما في ذلك الرأفة والوطنية والأخلاق والوحدة والشفافية والأمانة وتحمل المسؤولية واللغة الوطنية؛
- هـ. بناء المهارات الحياتية والمتصلة بالعمل من أجل زيادة الكفاءة في الحياة اليومية؛
- و. تطوير عادة الإعجاب بالعمل وتقييمه من أجل زيادة الإنتاجية والكفاءة في الإنتاج وتقديم الخدمات؛
- ز. تحديد القضايا الاجتماعية الشاملة والعناية بها، بما في ذلك صحة ورفاهية الأشخاص الآخرين (المجتمع) ، والمساواة الجنسية ، وكذلك إدارة البيئة والحفاظ عليها بشكل مستدام؛ و
- ح. تطوير التعاون الوطني والدولي والسلام والعدالة وفقا لدستور والاتفاقيات الدولية.

2.0 Malengo Makuu ya Elimu Tanzania

Malengo makuu ya elimu ni kumwezesha kila Mtanzania:

- (a) Kukuza na kuboresha haiba yake ili aweze kujithamini na kujiamini;
- (b) Kuheshimu utamaduni, mila na desturi za Tanzania, tofauti za kitamaduni, utu, haki za binadamu, mitazamo na matendo jumuishi;
- (c) Kukuza maarifa na kutumia sayansi na teknolojia, ubunifu, fikra tunduizi, uvumbuzi, ushirikiano, mawasiliano na mtazamo chanya katika maendeleo yake binafsi, na maendeleo endelevu ya taifa na dunia kwa ujumla;

- (d) Kuelewa na kulinda Tunu za Taifa ikiwa ni pamoja na utu, uzalendo, uadilifu, umoja, uwazi, uaminifu, uwajibikaji na lugha ya Taifa;
- (e) Kujenga štadi za maisha na štadi za kazi ili kuongeza ufanisi katika maisha ya kila siku;
- (f) Kukuza tabia ya kupenda na kuheshimu kazi ili kuongeza tija na ufanisi katika uzalishaji na utoaji wa huduma;
- (g) Kutambua na kuzingatia masuala mtambuka ambayo ni pamoja na afya na ustawi wa watu (jamii), usawa wa kijinsia, usimamizi na utunzaji endelevu wa mazingira; na
- (h) Kukuza ushirikiano wa kitaifa na kimataifa, amani na haki kwa kuzingatia Katiba ya nchi na mikataba ya kimataifa

3.0 أهداف التعليم للمرحلة الثانوية العامة

تتمثل أهداف التعليم للمرحلة الثانوية العامة في الآتي:

- (أ) تعزيز وتوسيع وتطوير الفهم العميق للمعارف والمهارات والتوجيهات التي حصل عليها في المرحلة الابتدائية؛
- (ب) حماية التقاليد والعادات، والوحدة الوطنية، والمقدرات الوطنية، والديمقراطية، وتقدير حقوق الإنسان والحقوق المدنية، والالتزامات والمسؤوليات المصاحبة لتلك الحقوق؛
- (ج) تنمية الثقة بالنفس والقدرة على التعلم في مختلف المجالات بما في ذلك العلوم والتكنولوجيا والمعرفة النظرية والتقنية؛
- (د) تعزيز التواصل باستخدام المهارات اللغوية، بما في ذلك لغة الإشارة في تنزانيا (LAT)؛ ولغة اللمس؛ واللغة السواحيلية والإنجليزية ولغة أجنبية واحدة أخرى على الأقل (اللغة العربية و اللغة الفرنسية و اللغة الصينية)
- (هـ) تعزيز المسؤولية في القضايا الاجتماعية الشاملة، بما في ذلك الصحة والأمن والسلامة والمساواة بين الجنسين وحماية بيئية مستدامة؛
- (و) بناء المعارف والمهارات المختلفة التي ستمكنه من العمل الحر (التوظيف الشخصي) والتوظيف وإدارة الحياة من خلال الاستخدام الجيد لبيئته، و
- (ز) تعزيز الاستعداد للتطوير الذاتي والتدريب على التعليم الثانوي والتعليم العالي.

3.0 Malengo ya Elimu ya Sekondari Kidato cha I–IV

Malengo ya Elimu ya Sekondari Kidato cha I–IV Elimu ya ni:

- (a) Kuimarisha, kupanua na kuendeleza uelewa wa kina wa maarifa, stadi na mwelekeo alioupata katika hatua ya elimu ya msingi;
- (b) Kulinda mila na desturi, umoja wa kitaifa, Tunu za Taifa, demokrasia, kuthamini haki za binadamu na za kiraia, wajibu na majukumu yanayoendana na haki hizo;
- (c) Kukuza tabia ya kujiamini na uwezo wa kujifunza kwenye nyanja mbalimbali zikiwemo sayansi na teknolojia, maarifa ya kinadharia, na kiufundi;
- (d) Kuimarisha mawasiliano kwa kutumia stadi za lugha ikiwemo Lugha ya Alama ya Tanzania (LAT), lugha mguso, lugha ya Kiswahili, Kiingereza na angalau lugha moja nyingine ya kigeni;
- (e) Kuimarisha uwajibikaji katika masuala mtambuka ya kijamii yakiwemo afya, usalama, usawa wa kijinsia na utunzaji endelevu wa mazingira;
- (f) Kujenga ujuzi na stadi mbalimbali zitakazomwezesha kujiajiri, kuajiriwa, na kuyamudu maisha kwa kutumia vizuri mazingira yake; na
- (g) Kukuza utayari wa kujiendeleza na mafunzo ya elimu ya kati na ya juu.

4.0 الكفايات العامة للتعليم الثانوية العامة

الكفاءة العامة التي سيبنيها طالب الثانوية العامة للصف I-VI هي:

(أ) توظيف المعارف والمهارات المكتسبة في مرحلة التعليم الابتدائي لتعزيز وتوسيع الفهم الأكاديمي؛

(ب) احترام المواطنة والعادات الوطنية؛

- (ج) إظهار الثقة في التعلم في مختلف المجالات بما في ذلك العلوم والتكنولوجيا والمعارف النظرية والتطبيقية والتقنية؛
- (د) توظيف المهارات اللغوية للتواصل، بما في ذلك لغة الإشارة في تنزانيا (LAT) ولغة الإشارة واللغة السواحيلية والانجليزية ولغة أجنبية واحدة أخرى على الأقل؛
- (هـ) استخدام المعرفة بالقضايا الشاملة لفهم البيئة المحيطة به؛ و
- (و) استخدام المعارف والمهارات لتمكينه من العمل الحر (التوظيف الشخصي) والتوظيف والقدرة على التعامل مع الحياة والبيئة.

4.0 Umahiri wa Jumla wa Elimu ya Sekondari Kidato cha I–IV

Umahiri wa jumla utakaojengwa na mwanafunzi wa Sekondari Kidato cha I–IV

- (a) Kutumia maarifa na štadi alizozipata katika hatua ya elimu ya msingi kuimarisha na kupanua uelewa wa masomo ya jumla;
- (b) Kuthamini uraia na Tunu za Taifa;
- (c) Kuonesha kujiamini katika kujifunza nyanja mbalimbali zikiwemo Sayansi na Teknolojia, maarifa ya kinadharia na kivitendo;
- (e) Kutumia štadi za lugha ikiwemo Lugha ya Alama ya Tanzania (LAT), lugha ya Kiswahili, Kiingereza na angalau lugha moja nyingine ya kigeni kuwasiliana;
- (f) Kutumia maarifa ya masuala mtambuka kuyamudu mazingira yanayomzunguka; na
- (g) Kutumia ujuzi na štadi kumwezesha kujiajiri, kuajiriwa na kuyamudu maisha na mazingira.

5.0 الكفاءات العامة والكفاءات الخاصة

الكفاءات الخاصة التي سيتم تطويرها موضحة في الجدول ١

5.0 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi

Muhtasari wa Lugha ya Kiarabu Sekondari Kidato cha I–IV una umahiri mkuu na umahiri mahususi kama inavyooneshwa katika Jedwali Na.1.

جدول رقم 1: الكفاءات العامة و الكفاءات الخاصة:

Jedwali Na 1: Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi kwa kidato cha I-IV

الكفاءات الخاصة Umahiri mahususi	الكفاءات العامة Umahiri mkuu
١,١ تطوير مهارات الاستماع اللغة العربية 1.1. Kukuza stadi za kusikiliza lugha ya Kiarabu	١.٠ إظهار فهم المهارات الأساسية للغة العربية 1.0 Kuonesha uelewa wa stadi za msingi za lugha ya Kiarabu
٢,١ اكتساب المفردات من المحادثة والكتابة 1.2 Kumudu msamiati kutokana na mazungumzo na maandishi	
٣,١ توصيل المعلومات الفصيحة القصيرة المنطوقة بكلمات فصيحة 1.3 Kuwasilisha ujumbe fasaha mfupi wa maneno kwa kutumia matamshi sahihi	

الكفاءات الخاصة Umahiri mahususi	الكفاءات العامة Umahiri mkuu
٤,١ استخدام المفردات والقواعد الصحيحة عن طريق التحدث والكتابة 1.4. Kutumia msamiati na sarufi sahihi katika mazungumzo na maandishi	
١,٢ تطوير كفاءة الاستماع وفهم المعلومات المعروضة شفويا 2.1. Kukuza umahiri wa kusikiliza na kuelewa taarifa zilizowasilishwa kwa mdomo	٠,٢ إظهار فهم المعلومات المعروضة شفويا وكتابيا 2. Kuonesha uelewa wa taarifa zilizowasilishwa kwa mdomo na kwa maandishi
٢,٢ تطوير كفاءة القراءة وفهم للنصوص المختلفة 2.2. Kukuza umahiri wa kusoma na kuelewa matini mbalimbali	
٣,٢ إظهار الاستجابة المناسبة في السياقات التواصلية المختلفة 2.3. Kuonesha mwitiko sahihi katika miktadha mbalimbali ya kimawasiliano	
٤,٢ تطوير كفاءة القراءة وفهم للنصوص المختلفة بشكل صحيح 2.4 Kukuza umahiri wa kusoma na kuelewa matini mbalimbali kwa usahihi	
١,٣ إنشاء النصوص باللغة الفصيحة في سياقات مختلفة 3.1. Kuunda matini fasaha katika miktadha mbalimbali	٠,٣ التواصل بفعالية في سياقات مختلفة 3.0 Kuwasiliana kwa ufanisi katika miktadha mbalimbali

الكفاءات الخاصة Umahiri mahususi	الكفاءات العامة Umahiri mkuu
١,٤ تقديم التفسير السهل الصحيح 4.1. Kutoa tafsiri sahili na sahihi	٤,٥ التفسير والتحرير والترجمة للمعلومات السهلة 4.0 Kutafsiri, kuhariri na kukalimani taarifa sahili
٢,٤ القدرة على تحرير النصوص السهلة 4.2. Kumudu uhariri wa matini sahili	
٣,٤ إجراء الترجمة السهلة بصورة صحيحة 4.3. Kumudu ukalimani sahili kwa usahihi	

6.0 دور المعلمين والطلاب والآباء في تعليم وتعلم

بشكل عام ، يتم توزيع أنشطة التعليمية والتعلمية الأساسية وفقاً للمعنيين الآتي ذكرهم:

6.0 Majukumu ya Mwalimu, Mwanafunzi na Mzazi/Mlezi katika Ufundishaji na Ujifunzaji

Ufundishaji na ujifunzaji unategemea ushirikiano madhubuti baina ya mwalimu, mwanafunzi na mzazi/mlezi. Majukumu yao ni kama yafuatayo:

6.1 المعلم

يرجى من المعلم

أ. تمكين الطالب من التعلم واكتساب الكفاءة المقصودة في اللغة العربية؛

ب. استخدام أساليب التعليم والتعلم على أساس العمر والقدرات والاحتياجات المختلفة التي يتمكن الطالب من

i - بناء الكفاءات المطلوبة في القرن الحادي والعشرين (21) ؛

ii - المشاركة بأكملها في عملية التعلم

ج. استخدام اساليب التشاركية التي تجعل الطالب مركز التعلم ، بما في ذلك التي ستمكنه من التفكير وطلب المعرفة من مصادر مختلفة

تشمل طرق المقترحة لتعلم وتعليم والبحث والتجارب العلمية والمناقشة وعمل المشروع التي تهدف إلى حل المشكلات الحقيقية في بيئة الطالب. بالإضافة إلى ذلك ، يتم تشجيع المعلم على استخدام مثل هذه أساليب أخرى وفقاً للسياق من أجل تحقيق بناء الكفاءة المقصود. تهيئة فصل آمن لذي بيئة ملائمة للتعليم والتعليم ؛

هـ. تطوير أدوات التعليم والتعلم وتقييمها

و. إجراء اختبار مستمر بانتظام باستخدام أدوات وأساليب الاختبار والتقييم التي تقيس النظرية والممارسة بما في ذلك العصف الذهني ، وقوائم المراجعة ، والاختبارات ، والاستبيانات ، والتمارين (العمل الفردي ، والعمل الجماعي) ، والمشروع و مَلَف. الأدوات والأساليب الأخرى هي الاختبارات العملية والعروض التقديمية وامتحانات منتصف الفصل والامتحانات النهائية؛

ز. التأكد من أن عملية التعلم والتعليم تتم بشكل عادل ومتساوٍ لكل طالب بغض النظر عن اختلافاتهم

ح. تحديد احتياجات الطالب وتقديم الحل المناسب؛

ط. حماية الطالب إذا كان في المدرسة

ي. تتبع التقدم اليومي للطالب

ك. إشراك الآباء / الأوصياء والمجتمع في عملية تعلم الطالب

ل. إدراج القضايا الشاملة وتكنولوجيا المعلومات والاتصالات في أنشطة التعليم والتعلم

6.1 Mwalimu

Mwalimu anatarajiwa:

- (a) Kumwezesha mwanafunzi kujifunza na kupata umahiri uliokusudiwa katika lugha ya Kiarabu;
- (b) Kutumia mbinu za kufundishia na kujifunzia kwa kuzingatia umri, mahitaji anuai, na uwezo wa mwanafunzi zitakazomwezesha:
 - i- Kujenga umahiri unaohitajika katika karne ya 21
 - ii- Kushiriki kikamilifu katika tendo zima la ujifunzaji
- (c) Kutumia mbinu shirikishi zinazomfanya mwanafunzi kuwa kitovu cha ujifunzaji zikiwemo zile zitakazomwezesha kufikiri, kutafakari na kutafuta maarifa kutoka katika vyanzo mbalimbali. Njia za kufundishia na kujifunzia zinazopendekezwa ni pamoja na kazi za vitendo, utafiti, majaribio ya kisayansi, majadiliano na kazi mradi zinazolenga kutatua matatizo halisi katika mazingira ya mwanafunzi. Aidha mwalimu anahimizwa kutumia njia nyingine kama hizo kulingana na muktadha ili kufanikisha ujenzi wa umahiri uliokusudiwa.
- (d) Kuandaa darasa salama lenye mazingira rafiki ya kufundishia na kujifunzia;
- (e) Kutengeneza na kufaragua zana za kufundishia na kujifunzia;
- (f) Kufanya upimaji endelevu mara kwa mara kwa kutumia zana na mbinu za upimaji na tathmini zinazopima nadharia na vitendo zikiwemo bunguabongo, orodhahakiki, majaribio, dodoso, maswali ya ana kwa ana, mazoezi, kazi kwa vitendo (kazi binafsi, kazi za vikundi), kazimradi na mkoba wa kazi. Zana na mbinu nyingine ni majaribio kwa vitendo, uwasilishaji, mitihani ya muhula na mtihani wa mwisho;
- (g) Kuhakikisha kuwa tendo la ujifunzaji na ufundishaji linafanyika kwa haki na usawa kwa kila mwanafunzi bila kujali tofauti zao;
- (h) Kumlinda mwanafunzi awapo shuleni;
- (i) Kufuatilia maendeleo ya mwanafunzi ya kila siku;
- (j) Kubaini mahitaji ya mwanafunzi na kutoa afua stahiki;
- (k) Kushirikisha wazazi/walezi na jamii katika hatua mbalimbali za ujifunzaji wa mwanafunzi;na
- (l) Kuchopeka masuala mtambuka na TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji

6.2 الطالب

يتوقع من الطالب:

- أ. أن يكون الرئيس التنفيذي في عملية التعلم بأكملها
- ب. لاكتساب الكفاءة المقصودة من خلال المشاركة في أنشطة التعلم المختلفة داخل الفصل وخارجه؛ و
- ج. المشاركة في العثور على المعرفة من مصادر مختلفة بما في ذلك الكتب المدرسية والملاحق والمنشورات الأخرى من المكتبة الإلكترونية

6.2 Mwanafunzi

Mwanafunzi anatarajiwa:

- (a) Kuwa mtendaji mkuu katika mchakato wote wa ujifunzaji;
- (b) Kupata umahiri unaokusudiwa kwa kushiriki katika shughuli mbalimbali za ujifunzaji ndani na nje ya darasa
- (c) Kushiriki katika kutafuta maarifa kutoka katika vyanzo mbalimbali ikiwemo vitabu vya kiada, ziada na machapisho mengine kutoka katika maktaba mtandao;

6.3 الوالد / الوصي

من المتوقع من الوالد / الوصي

- أ. الإشراف ومتابعة تقدم الولد في التعلم
- ب. الإشراف على الولد لأداء واجباته المهنية حيثما أمكن
- ج. التأكد من أن بيئة المنزل صديقة وآمنة تسهل التعلم
- د. تتبّع و مراقبة سلوك الولد
- هـ. تزويد الولد بجميع المواد المطلوبة في عملية التعلم
- و. التأكد من أن الولد يحصل على الاحتياجات اللازمة
- ز. توعية الولد بأهمية التعليم وقيّمته وتشجيعه على التعليم الجاد

6.3 Mzazi/Mlezi

Mzazi anatarajiwa:

- (a) Kusimamia na kufuatilia maendeleo ya mtoto katika ujifunzaji;
- (b) Kumsimamia mtoto kutekeleza kazi zake za kitaaluma pale inapowezekana;
- (c) Kuhakikisha kuwa mazingira ya nyumbani ni rafiki na salama yanayowezesha ujifunzaji;
- (d) Kufuatilia mwenendo wa kitabia wa mtoto;
- (e) Kumpatia mtoto vifaa vyote vinavyohitajika katika shughuli ya ujifunzaji;Kuhakikisha mtoto anapata mahitaji muhimu; na
- (g) Kumfundisha mtoto juu ya umuhimu na thamani ya elimu pamoja na kumuhimiza kujifunza kwa bidii.

7.0 أساليب التدريس المقترحة

تعتبر أساليب التعليم والتعلم أساسية في بناء الكفاءة لدى الطالب. يقترح هذا المقرر أساليب التعليم والتعلم لكل نشاط؛ منها الزيارات الأكاديمية، والأعمال، والسرود، والمناقشات، والتفكير، والكتابة، والمشاركة الزوجية، وعمل المشروع. ومع ذلك، يُنصح المعلم باستخدام أساليب أخرى من هذا القبيل اعتمادًا على سياق التعليم والتعلم.

7.0 Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji

Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji ni msingi katika kujenga umahiri kwa mwanafunzi. Muhtasari huu unapendekeza mbinu za ufundishaji na ujifunzaji kwa kila shughuli. Miongoni mwa mbinu hizo ni ziara za kimasomo, kazi za vitendo, masimulizi, majadiliano, fikiri-andika-jozisha-shirikisha na kazimradi. Hata hivyo, mwalimu anashauriwa kutumia mbinu nyingine kama hizo kulingana na muktadha wa ufundishaji na ujifunzaji.

8.0 الوسائل التعليمية المقترحة

تتطلب عملية التعليم والتعلم أدوات أو معدات مختلفة لبناء الكفاءة المقصودة. وبالتالي، يجب على المعلم والطالب التعاون في إعداد أو اختيار أدوات أو معدات متوفرة في بيئة المدرسة والمنزل عند الحاجة. يجب على المعلم والطالب السعي للحصول على المعلومات من مصادر مختلفة لتحقيق الكفاءة في عملية التعليم والتعلم. ستقدم TET قائمة بمصادر أو معدات المعتمدة للاستخدام كمرجع.

8.0 Zana za ufundishaji na ujifunzaji

Mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji unahitaji zana/vifaa mbalimbali ili kujenga umahiri uliokusudiwa. Hivyo, mwalimu na mwanafunzi wanapaswa kushirikiana katika kuandaa au kufaragua zana/vifaa mbadala vinavyopatikana katika mazingira ya shuleni na nyumbani pindi vinapohitajika. Mwalimu na mwanafunzi wanapaswa kutafuta taarifa kutoka katika vyanzo mbalimbali ili kuleta ufanisi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Orodha ya vitabu vilivyoidhinishwa kutumika kwa ajili ya rejea vitatolewa na TET.

9.0 قياس تقدم التعلم

تعد عملية قياس تقدم التعلم قضية مهمة في عملية التعليم والتعلم. سيتم قياس اللغة العربية بالتوازي مع المواد الأخرى التي تدرّس في المرحلة الثانوية العامة من الصف الأول إلى الرابع. ستمكّن عملية القياس المعلم من معرفة قدرة الطالب في الاستماع، والكتابة، والقراءة، والتحدث بفصاحة وطلاقة في المواقف الحياتية المتنوعة، والإجابة عن الأسئلة حول المعلومات التي قرأها أو استمع إليها، وكتابة الأخبار أو القصص في موضوعات مختلفة. إضافة إلى ذلك، ستمكّن عملية التقييم المعلم من تحديد قدرة الطالب في استخدام المفردات المناسبة في سياقات مختلفة من الكتابة والمحادثة. يعتمد تقييم تقدم الطالب على المعايير المحددة في كل نشاط تعليمي؛ لذلك، فإن الأدوات المستخدمة في الاختبار تشمل التمارين، والأسئلة الشفوية المباشرة، والملاحظة الدقيقة، والاختبارات، والاستبانات، وحقبة العمل، والمشاريع، وامتحانات الفصل الدراسي، بالإضافة إلى تصميم وتأليف الأعمال المتنوعة.

بالإضافة إلى ذلك، يرتبط القياس بالتقييم التكويني والتقييم النهائي حيث يساهم التقييم التكويني 30% بينما التقييم النهائي للصف الرابع 70%. من جانب التقييم التكويني، علامات التقييم تصدر من التقييم الوطني للصف السادس الابتدائي (7.5%)، والتقييم الوطني للصف الثاني الثانوي (7.5%)، والامتحان الأخير للصف الثالث الثانوي (5%)، وعمل مشروع آخر الصف الثالث الثانوي (5%) والاختبار التجريبي للصف الرابع الثانوي (5%). توزيع هذه العلامات يوضح في الجدول رقم 2

9.0 Upimaji wa Maendeleo ya Ujifunzaji

Upimaji wa maendeleo ya ujifunzaji ni suala muhimu katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Upimaji wa Lugha ya Kiarabu utafanyika sambamba na masomo mengine yanayofundishwa katika ngazi ya Sekondari Kidato cha I-IV. Upimaji huu unamwezesha mwalimu kupima umahiri wa mwanafunzi wa kusikiliza, kuzungumza, kusoma, na kuandika kwa ufasaha katika miktadha mbalimbali, kujibu maswali ya habari aliyoisoma au kuisikiliza, kubuni kazi mbalimbali, kutafsiri, kukalimani, na kuhariri. Aidha, unamwezesha mwalimu kubaini uwezo wa mwanafunzi wa kutumia msamiati sahihi katika miktadha mbalimbali ya uandishi na mazungumzo. Upimaji wa maendeleo ya mwanafunzi utazingatia vigezo vilivyoainishwa katika kila shughuli ya ujifunzaji. Kwa hiyo, zana zinazotumika katika upimaji ni pamoja na mazoezi, maswali ya ana kwa ana, orodha hakiki, majaribio, uchunguzi, hojaji, mkoba wa kazi, kazi mradi na mitihani.

Aidha, upimaji utahusisha upimaji endelevu na upimaji wa mwisho ambapo upimaji endelevu utachangia aslimia 30 ya upimaji wote na upimaji wa mwisho wa kuhitimu Kidato cha Nne utabeba asilimia 70. Kwa upande wa upimaji endelevu, alama za upimaji endelevu zitatokana na Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Sita (7.5%), Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili (7.5%), mtihani wa muhula wa mwisho wa Kidato cha Tatu (5%), kazimradi (project) inayofanyika mwishoni mwa Kidato cha Tatu (5%), na mtihani wa utamilifu (mock) wa Kidato cha Nne (5%). Mgawanyo wa alama hizi unaoneshwa katika Jedwali Na. 2.

جدول رقم 2: توزيع علامات التقييم

Jedwali Na. 2: Mgawanyo wa Alama za Upimaji

Na	Upimaji القياس	العلامات (%) Alama
1.	التقييم الوطني للصف السادس الابتدائي Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Sita	7.5
2.	التقييم الوطني للصف الثاني الثانوي Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili	7.5
3.	الاختبار النهائي للصف الثالث الثانوي Mtihani wa muhula wa mwisho wa Kidato cha Tatu	5
4.	عمل مشروع آخر للصف الثالث الثانوي Kazimradi inayofanyika mwishoni mwa Kidato cha Tatu	5
5.	الاختبار التجريبي للصف الرابع الثانوي Mtihani wa utamilifu wa Kidato cha Nne	5
6.	الامتحان الشهادة للصف الرابع الثانوي Mtihani wa kuhitimu Kidato cha Nne	70
المجموع الكلي Jumla		100

10.0 عدد الحصص

يقدم مقرر اللغة العربية للتعليم الثانوية المتوسطة تقديرات للوقت الذي سيتم قضاؤه في التعليم والتعلم. نظرًا لكثرة الكفاءات الخاصة وأنشطة التعلم، تم تخصيص حصتين في الأسبوع للمرحلة الثانوية، لكل منهما أربعون دقيقة.

10.0 Idadi ya Vipindi

Muhtasari wa Kiarabu Sekondari Kidato cha I–IV unatoa makadirio ya muda utakaotumika katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia uzito wa umahiri mahususi na shughuli za kutendwa na mwanafunzi. Makadirio haya ya muda yamewekwa kwa mfumo wa vipindi, ambapo kila kipindi ni dakika 40. Idadi ya vipindi kwa somo hili ni viwili (2) kwa wiki kwa kidato cha I–IV.

11.0 محتوى التعليم والتعلم.

يحتوي مقرر اللغة العربية للصف الأول الثانوي إلى الصف الرابع على محتوى منظم في سبعة عناصر متمثلة في الكفاية العامة، والكفاية الخاصة، وأنشطة الطالب، والأساليب المقترحة، ومعايير التقييم، والوسائل التعليمية والتعلمية، بالإضافة إلى عدد الحصص موضحة في الجدول أدناه.

11.0 Maudhui ya Ufundishaji na Ujifunzaji

Muhtasari wa Kiarabu Sekondari Kidato cha I–IV umebeba maudhui ambayo yamepangiliwa katika vipengele saba, ambavyo ni umahiri mkuu, umahiri mahususi, shughuli za ujifunzaji, mbinu pendekezwa, vigezo vya upimaji, zana/vifaa pamoja na idadi ya vipindi kama inavyooneshwa katika jedwali hapo chini.

Jedwali Na 3: Maudhui ya Kidato cha I

عدد الحصص Idadi ya vipindi	الوسائل التعليمية و التعليمية Zana za ufundishaji na ujifunzaji	معايير التقييم Vigezo vya upimaji	الأساليب المقترحة Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	الأنشطة التعليمية Shughuli za ujifunzaji	الكفاءات الخاصة Umahiri mahususi	الكفاءات العامة Umahiri mkuu
12	المسجلات الصوتية المتخصصة في مهارة الاستماع Vinasa sauti vyenye mada au maudhui ya kusikiliza	تم الاستماع للفهم إلى نصوص قصيرة سهلة بطريقة جيدة Matini fupi sahili zimesikilizwa kwa umakini	القصة: أرشد الطلاب إلى الاستماع للنصوص القصيرة السهلة بطريقة صحيحة. Kisa: Waongoze wanafunzi kusikiliza habari fupi sahili kwa usahihi المنافشة الجماعية: ساعد الطلاب على مناقشة النصوص القصيرة المقروءة وتعيين الأفكار الرئيسية Majadiliano ya vikundi: Wasaidie wanafunzi kujadili matini fupi iliyosomwa na kubainisha wazo kuu	(أ) الاستماع للفهم إلى نصوص قصيرة سهلة (a) Kusikiliza kwa ufahamu matini fupi sahili	1.1 تنمية مهارات الاستماع اللغة العربية 1.1 Kukuza stadi za kusikiliza Kiarabu	1.0 إظهار فهم المهارات الأساسية للغة العربية 1.0 Kuonesha uelewa wa stadi za msingi za lugha ya Kiarabu

عدد الحصص Idadi ya vipindi	الوسائل التعليمية و التعليمية Zana za ufundishaji na ujifunzaji	معايير التقييم Vigezo vya upimaji	الأساليب المقترحة Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	الأنشطة التعليمية Shughuli za ujifunzaji	الكفاءات الخاصة Umahiri mahususi	الكفاءات العامة Umahiri mkuu
	مسجلات الصوتية المتخصصة في مهارة الاستماع Vinasa sauti vyenye mada au maudhui ya kusikiliza	تمت مناقشة الرسالة من نصوص قصيرة Ujumbe unaopatikana katika matini fupi umejadiliwa	المناقشة الجماعية: وجه الطلاب إلى مناقشة الرسالة من النصوص القصيرة Majadiliano ya vikundi: Waongoze wanafunzi kujadili ujumbe unaopatikana katika matini fupi فكر – اكتب- زوج – أشرك: أرشد الطلاب إلى الإجابة عن الأسئلة ومشاركة زملائهم في تقديم رسالة النص Fikiri-andika jozisha- shirikisha: Waongoze wanafunzi kujibu maswali na kushirikiana na wenzao katika kuwasilisha ujumbe unaopatikana katika matini	(ب) مناقشة الرسالة من نصوص قصيرة سهلة (b) Kujadili ujumbe unaopatikana katika matini fupi sahili		

عدد الحصص Idadi ya vipindi	الوسائل التعليمية و التعليمية Zana za ufundishaji na ujifunzaji	معايير التقييم Vigezo vya upimaji	الأساليب المقترحة Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	الأنشطة التعليمية Shughuli za ujifunzaji	الكفاءات الخاصة Umahiri mahususi	الكفاءات العامة Umahiri mkuu
			<p>Majadiliano ya vikundi: Wasaidie wanafunzi kujadili habari waliyoisikiliza na kubaini mawazo makuu</p> <p>التأمل الذاتي: وجّه الطلاب إلى التمييز بين أنواع مختلفة من الكلمات من النصوص المسموعة</p> <p>Tafakuri binafsi: Waelekeze wanafunzi kujadili kwa kuhusianisha na kutofautisha aina mbalimbli za maneno katika habari walioisikiliza.</p>			

عدد الحصص Idadi ya vipindi	الوسائل التعليمية و التعليمية Zana za ufundishaji na ujifunzaji	معايير التقييم Vigezo vya upimaji	الأساليب المقترحة Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	الأنشطة التعليمية Shughuli za ujifunzaji	الكفاءات الخاصة Umahiri mahususi	الكفاءات العامة Umahiri mkuu
14	الوسائل السمعية البصرية Zana au vifaa vya masikiziuoni vyenye mada au maudhui ya kusikiliza	تم الاستماع إلى النصوص السهلة القصيرة المتعلقة بحقوق الانسان وبيان معاني المفردات الجديدة منها Matini fupi na nyepesi kuhusu haki za binadamu imesikilizwa, na maana ya maneno mapya katika matini yamebainishwa kwa usahihi	العمل الجماعي: وجّه الطلاب إلى الإجابة عن الأسئلة من النصوص القصيرة Kazi ya vikundi: Waongoze wanafunzi kujibu maswali kutoka katika matini fupi waliosikiliza. حل المشكلة: وجّه الطلاب إلى البحث عن معاني المفردات الجديدة الواردة من النصوص القصيرة التي استمعوا إليها Utatuzi wa tatizo: Waongoze wanafunzi kutafiti maana ya msamiati kutoka katika matini fupi waliosikiliza.	(أ) الاستماع إلى نصوص قصيرة سهلة متعلقة بحقوق الإنسان وبيان معاني الكلمات الجديدة منها (a) Kusikiliza nakubaini maneno mapya katika matini kuhusu haki za binadamu	1.2 اكتساب المفردات من المحادثة والكتابة 1.2 Kumudu msamiati kutokana na mazungumzo na maandishi	

عدد الحصص Idadi ya vipindi	الوسائل التعليمية و التعليمية Zana za ufundishaji na ujifunzaji	معايير التقييم Vigezo vya upimaji	الأساليب المقترحة Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	الأنشطة التعليمية Shughuli za ujifunzaji	الكفاءات الخاصة Umahiri mahususi	الكفاءات العامة Umahiri mkuu
			<p>زيارة في القاعة: وجه الطلاب إلى التعرف على أنواع مختلفة من المفردات ومناقشتها مع زملائهم.</p> <p>Matembezi ya galari: Waongoze wanafunzi kubaini aina za msamiati na kujadili baina yao</p>			
	<p>النصوص المختلفة المتخصصة في موضوع المفردات</p> <p>Matini anuai zenye mada ya msamiati</p>	<p>تمَّ استخدام المفردات الجديدة المكتسبة في المحادثة والكتابة استخداما صحيحا</p> <p>Maneno mapya aliyobaini katika mazungumzo na maandishi yametumiwa kwa usahihi</p>	<p>حلّ المشكلة : مكن الطلاب من استخدام المفردات الجديدة المكتسبة من النصوص المقروءة والمسموعة في جمل مفيدة متنوعة.</p> <p>Utatuzi wa tatizo: Wawezeshe wanafunzi kutumia msamiati mpya walioupata katika mazungumzo na mandishi katika sentensi mbalimbali.</p>	<p>(ب) استخدام المفردات التي بينها في المحادثة والكتابة</p> <p>(b) Kutumia msamiati aliyobaini katika mazungumzo na maandishi</p>		

عدد الحصص Idadi ya vipindi	الوسائل التعليمية و التعليمية Zana za ufundishaji na ujifunzaji	معايير التقييم Vigezo vya upimaji	الأساليب المقترحة Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	الأنشطة التعليمية Shughuli za ujifunzaji	الكفاءات الخاصة Umahiri mahususi	الكفاءات العامة Umahiri mkuu
16	النصوص المتنوعة عن موضوعات التواصل الشفوي Matini mbalimbali zenye maudhui ya uwasilishaji kwa njia ya masimulizi ya mdomo	تم تقديم الاقتراحات كتابة وشفاهة في سياقات مختلفة (مثل: المستشفى، والمكتبة، وموقف السيارات Maoni kwa mdomo katika miktadha mbalimbali yametolewa (mfano: hospitali, maktaba, na maegesho ya magari)	دراسة حالة: أرشد الطلاب إلى تقديم الاقتراحات في سياقات مختلفة. Kisamafunzo: Waelekeze wanafunzi kutoa maoni kwa mdomo katika miktadha mbalimbali. المناقشة الجماعية: مكّن الطلاب من مناقشة أنواع مختلفة من اقتراحات مقدمة في سياقات مختلفة. Majadiliano ya vikundi: Waongoze wanafunzi kujadili maoni mbalimbali yaliyotolewa katika miktadha mbalimbali.	(أ) تقديم الاقتراحات شفاهة في سياقات مختلفة (a) Kutoa maoni kwa mdomo katika miktadha mbalimbali	1.3 توصيل المعلومات الفصيحة القصيرة المنطوقة بكلمات فصيحة 1.3 Kuwasilisha ujumbe fasaha mfupi wa maneno kwa kutumia matamshi sahihi	

عدد الحصص Idadi ya vipindi	الوسائل التعليمية و التعليمية Zana za ufundishaji na ujifunzaji	معايير التقييم Vigezo vya upimaji	الأساليب المقترحة Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	الأنشطة التعليمية Shughuli za ujifunzaji	الكفاءات الخاصة Umahiri mahususi	الكفاءات العامة Umahiri mkuu
			<p>الحوار: مكّن الطلاب من المشاركة في حوارات ذات سياقات مختلفة وتقديم مقترحات متنوعة.</p> <p>Dayalojia: Wawezeshe wanafunzi kushiriki katika dayalojia katika miktadha mbalimbali na kutoa maoni yao</p>			
	<p>النصوص المتنوعة عن موضوعات التواصل الشفوي</p> <p>Matini mbalimbali zenye maudhui ya uwasilishaji kwa njia ya masimulizi ya mdomo</p>	<p>تمّ التعبير عن الأحداث المسموعة أو المشهودّة المختلفة</p> <p>Matukio mbalimbali yaliyoonekana na wanafunzi au kusikilizwa yameelezwa kwa usahihi</p>	<p>دراسة حالة: أرشد الطلاب إلى تقديم الاقتراحات في سياقات مختلفة شفويًا.</p> <p>Masimulizi: Waelekeze wanafunzi kutoa maoni kwa mdomo katika miktadha mbalimbali.</p>	<p>(ب) التعبير عن الأحداث التي شاهدها أو سمعها بطريقة فصيحة</p> <p>(b) Kuelezea kwa ufasaha matukio mbalimbali aliyoyaona au kuyasikia</p>		

عدد الحصص Idadi ya vipindi	الوسائل التعليمية و التعليمية Zana za ufundishaji na ujifunzaji	معايير التقييم Vigezo vya upimaji	الأساليب المقترحة Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	الأنشطة التعليمية Shughuli za ujifunzaji	الكفاءات الخاصة Umahiri mahususi	الكفاءات العامة Umahiri mkuu
			<p>المناقشة الجماعية: مكّن الطلاب من مناقشة أنواع مختلفة من اقتراحات مقدمة في سياقات مختلفة.</p> <p>Majadiliano ya vikundi: Waongoze wanafunzi kujadili maoni mbalimbali yaliyotolewa katika miktadha mbalimbali.</p> <p>الحوار: مكّن الطلاب من المشاركة في حوارات ذات سياقات مختلفة وتقديم مقترحات متنوعة.</p> <p>Dayalojia: Wawezeshe wanafunzi kushiriki katika dayalojia katika miktadha mbalimbali na kutoa maoni yao</p>			

عدد الحصص Idadi ya vipindi	الوسائل التعليمية و التعليمية Zana za ufundishaji na ujifunzaji	معايير التقييم Vigezo vya upimaji	الأساليب المقترحة Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	الأنشطة التعليمية Shughuli za ujifunzaji	الكفاءات الخاصة Umahiri mahususi	الكفاءات العامة Umahiri mkuu
8	النصوص المختلفة ذات موضوعات سردي شفهي Matini anuai zenye maudhui ya masimulizi ya mdomo (mazungumzo) na maandishi	تمّ استخدام أنواع مختلفة لأخبار المبتدأ في المحادثة والكتابة متنوعة Aina mbalimbali za viarifu zimetumiwa katika mazungumzo na maandishi	المشروع: مكّن الطلاب من التعرف على أنواع متعددة من أخبار المبتدأ. Kazimradi: Waongoze wanafunzi kutambua aina mbalimbali za viima. المناقشة الجماعية: أرشد الطلاب إلى مناقشة أنواع متنوعة من أخبار المبتدأ. Majadiliano ya vikundi: Waelekeze wanafunzi kujadili aina mbalimbali za viarifu.	(أ) استخدام أنواع مختلفة لأخبار المبتدأ في المحادثة والكتابة في سياقات مختلفة (a) Kutumia aina mbalimbali za viarifu katika mazungumzo na maandishi katika miktadha mbalimbali	٤, ١ استخدام المفردات والقواعد الصحيحة كتابة وشفاهة 1.4 Kutumia msamiati na sarufi sahihi katika mazungumzo na maandishi	

عدد الحصص Idadi ya vipindi	الوسائل التعليمية و التعليمية Zana za ufundishaji na ujifunzaji	معايير التقييم Vigezo vya upimaji	الأساليب المقترحة Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	الأنشطة التعليمية Shughuli za ujifunzaji	الكفاءات الخاصة Umahiri mahususi	الكفاءات العامة Umahiri mkuu
			<p>حلُّ المشكلة: وجه الطلاب إلى استخدام أنواع مختلفة من أخبار المبتدأ في سياقات متنوعة شفاهة وكتابة.</p> <p>Utatuzi wa tatizo: Waongoze wanafunzi kutumia aina mbalimbali za viarifu katika miktadha tofauti katika mazungumzo na maandishi.</p>			

عدد الحصص Idadi ya vipindi	الوسائل التعليمية و التعليمية Zana za ufundishaji na ujifunzaji	معايير التقييم Vigezo vya upimaji	الأساليب المقترحة Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	الأنشطة التعليمية Shughuli za ujifunzaji	الكفاءات الخاصة Umahiri mahususi	الكفاءات العامة Umahiri mkuu
8	النصوص المتنوعة والوسائل السمعية البصرية Matini mbalimbali na vifaa vya masikizi uoni	تم تبيين الرسالة من النصوص الطويلة السهلة بطريقة جيدة Ujumbe alioupata katika matini umeelezwa kwa usahihi	فكر – اكتب- زوج- أشرك: مكن الطلاب من التعرف على رسالة من النص الطويل البسيط Fikiri-andika –jozisha – shirikisha: Waongoze wanafunzi kubaini ujumbe unaopatikana katika matini ndefu sahili المناقشة الجماعية: سهل للطلاب مناقشة الرسالة من النصوص الطويلة السهلة. Majadiliano katika vikundi: Wasaidie wanafunzi kujadili ujumbe unaopatikana katika matini ndefu sahili	(أ) توضيح الرسالة الواردة في النص الطويل البسيط الذي استمع إليه (a) Kueleza ujumbe uliomo katika matini ndefu sahili aliyosikiliza	١,٢ تطوير كفاءة الاستماع وفهم المعلومات المعروضة شفويا 2.1 Kukuza umahiri wa kusikiliza na kuelewa taarifa zinazowasilishwa kwa mdomo	2.0 إظهار فهم المعلومات المعروضة شفويا وكتابيا 2.0 Kuonesha uelewa wa taarifa zilizo wasilishwa kwa mdomo na kwa maandishi

عدد الحصص Idadi ya vipindi	الوسائل التعليمية و التعليمية Zana za ufundishaji na ujifunzaji	معايير التقييم Vigezo vya upimaji	الأساليب المقترحة Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	الأنشطة التعليمية Shughuli za ujifunzaji	الكفاءات الخاصة Umahiri mahususi	الكفاءات العامة Umahiri mkuu
12	نصوص مختلفة متخصصة في القراءة Matini mbalimbali zenye maudhui ya kusoma	تمت قراءة النصوص المختلفة للفهم قراءة صحيحة Matini mbalimbali zimesomwa kwa ufahamu	العمل الجماعي: وجّه الطلاب إلى قراءة للفهم النصوص القصيرة السهلة Kazi za vikundi: Waelekeze wanafunzi kusoma kwa ufahamu matini fupi sahili لعِب الأدوار: وجّه الطلاب إلى بيان مفهوم النصوص القصيرة السهلة المقروءة. Igizodhima: Waongoze wanafunzi kubaini ufahamu wa matini fupi na sahili walioisoma.	(أ) قراءة للفهم النصوص المختلفة Kusoma kwa ufahamu matini mbalimbali	٢,٢ تطوير كفاءة القراءة وفهم للنصوص المختلفة 2.2 Kukuza umahiri wa kusoma na kuelewa matini mbalimbali	

عدد الحصص Idadi ya vipindi	الوسائل التعليمية و التعليمية Zana za ufundishaji na ujifunzaji	معايير التقييم Vigezo vya upimaji	الأساليب المقترحة Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	الأنشطة التعليمية Shughuli za ujifunzaji	الكفاءات الخاصة Umahiri mahususi	الكفاءات العامة Umahiri mkuu
	نصوص مختلفة متخصصة في القراءة Matini mbalimbali zenye maudhui ya kusoma	تم تعيين الفكرة الرئيسية من النصوص المقروءة بطريقة صحيحة Wazo kuu kutokana na matini zilizosomwa limeelezwa kwa usahihi	العمل الجماعي: ممكن الطلاب من تحديد الأفكار الرئيسية من النصوص المقروءة. Kazi za vikundi: Wawezeshe wanafunzi kuainisha mawazo makuu katika matini waliosoma. المنافسة الجماعية: ساعد الطلاب في توضيح الأفكار الرئيسية من النصوص المقروءة. Majadiliano ya vikundi: Waongoze wanafunzi kuchambua mawazo makuu katika matini walioisoma. حل المشكلة وجه الطلاب على ترتيب الأفكار الرئيسية من النصوص المقروءة.	(ب) توضيح الفكرة الرئيسية من النصوص المقروءة (b) Kueleza wazo kuu kutokana na matini aliosoma		

عدد الحصص Idadi ya vipindi	الوسائل التعليمية و التعليمية Zana za ufundishaji na ujifunzaji	معايير التقييم Vigezo vya upimaji	الأساليب المقترحة Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	الأنشطة التعليمية Shughuli za ujifunzaji	الكفاءات الخاصة Umahiri mahususi	الكفاءات العامة Umahiri mkuu
			Utatuzi wa tatizo Waelekeze wanafunzi kupangilia mawazo makuu katika matini walioisoma.			
	نصوص مختلفة متخصصة في مهارة القراءة Matini mbalimbali zenye maudhui au stadi za kusoma	تمت قراءة النصوص وتلخيصها كتابة Matini zimesomwa na kufupishwa kwa maandishi kwa usahihi	العمل الجماعي: مكّن الطلاب من تحديد الأفكار الرئيسية من النصوص المقروءة. Kazi za vikundi: Wawezeshe wanafunzi kuainisha mawazo makuu katika matini waliosoma. المناقشة الجماعية: ساعد الطلاب في توضيح الأفكار الرئيسية من النصوص المقروءة. Majadiliano ya vikundi: Waongodze wanafunzi kuchambua mawazo makuu katika matini walioisoma.	(ج) قراءة النصوص وتلخيص الرسالة من خلالها كتابة (c) Kusoma na kufupisha matini kwa maandishi		

عدد الحصص Idadi ya vipindi	الوسائل التعليمية و التعليمية Zana za ufundishaji na ujifunzaji	معايير التقييم Vigezo vya upimaji	الأساليب المقترحة Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	الأنشطة التعليمية Shughuli za ujifunzaji	الكفاءات الخاصة Umahiri mahususi	الكفاءات العامة Umahiri mkuu
			<p>حل المشكلة : وجّه الطلاب على تلخيص النصوص المقروءة.</p> <p>Utatuzi wa tatizo: Waelekeze wanafunzi kufupisha matini walioisoma.</p>			

Jedwali Na 4: Maudhui ya Kidato cha II

عدد الحصص Idadi ya vipindi	الوسائل التعليمية و التعليمية Zana za ufundishaji na ujifunzaji	معايير التقييم Vigezo vya upimaji	الأساليب المقترحة Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	الأنشطة التعليمية Shughuli za ujifunzaji	الكفاءات الخاصة Umahiri mahususi	الكفاءات العامة Umahiri mkuu
12	مسجلات الصوتية المختلفة المتخصصة في الاستماع Vinasa sauti anuai vyenye mada au maudhui ya kusikiliza	تم الاستماع للفهم إلى نصوص قصيرة مركبة Matini fupi changamani zimesikilizwa kwa ufahamu	المشهد: أرشد الطلاب إلى الاستماع للفهم النصوص القصيرة المركبة Tukio: Waongoze wanafunzi kusikiliza kwa ufahamu matini fupi changamani المناقشة الجماعية: وجّه الطلاب إلى مناقشة الأفكار الرئيسية من النص المسموع	(أ) الاستماع للفهم إلى النصوص القصيرة المركبة (a) Kusikiliza kwa ufahamu matini fupi changamani	1.1 تنمية مهارات استماع اللغة العربية 1.1 Kukuza stadi za kusikiliza Kiarabu	1.0 إظهار فهم المهارات الأساسية في اللغة العربية 1.0 Kuonesha uelewa wa stadi za msingi za lugha ya Kiarabu

عدد الحصص Idadi ya vipindi	الوسائل التعليمية و التعليمية Zana za ufundishaji na ujifunzaji	معايير التقييم Vigezo vya upimaji	الأساليب المقترحة Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	الأنشطة التعليمية Shughuli za ujifunzaji	الكفاءات الخاصة Umahiri mahususi	الكفاءات العامة Umahiri mkuu
			<p>Majadiliano ya vikundi: Waelekeze wanafunzi kujadili mawazo makuu kutoka katika matini walioisikiliza</p> <p>لعِب الأَدوار: وجه الطلاب إلى التعبير عما فهموا من النص الذي استمعوا إليه</p> <p>Igizodhima: Waongoze wanafunzi kueleza walichokielewa katika matini waliosikiliza</p>			

عدد الحصص Idadi ya vipindi	الوسائل التعليمية و التعليمية Zana za ufundishaji na ujifunzaji	معايير التقييم Vigezo vya upimaji	الأساليب المقترحة Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	الأنشطة التعليمية Shughuli za ujifunzaji	الكفاءات الخاصة Umahiri mahususi	الكفاءات العامة Umahiri mkuu
		تمت مناقشة الرسالة من نصوص Ujumbe unaopatikana katika matini umejadiliwa vyema	المناقشة الجماعية : أرشد الطلاب إلى مناقشة الرسالة من النص Majadiliano ya vikundi: Waongoze wanafunzi kujadili ujumbe unaopatikana katika matini فكر - اكتب - زوج - أشرك: أرشد الطلاب إلى الإجابة عن الأسئلة وإشراك زملائهم في تقديم الرسالة الواردة من النصوص القصيرة المركبة	(ب) مناقشة الرسالة وجدت في نصوص قصيرة مركبة (b) Kujadili ujumbe unaopatikana katika matini fupi changamani		

عدد الحصص Idadi ya vipindi	الوسائل التعليمية و التعليمية Zana za ufundishaji na ujifunzaji	معايير التقييم Vigezo vya upimaji	الأساليب المقترحة Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa	الأنشطة التعليمية Shughuli za ujifunzaji	الكفاءات الخاصة Umahiri mahususi	الكفاءات العامة Umahiri mkuu
			<p>Fikiri-andika-jozisha-shirikisha: Waongoze wanafunzi kujibu maswali na kushirikiana na wenzao katika kuwasilisha ujumbe unaopatikana katika matini fupi changamani</p>			

